

**BIKIRA MARIA WA  
MLIMA KARMELI**

# **JUMUIYA YA ROZARI HAI ULIMWENGUNI-TANZANIA**

## **NOVENA YA BIKIRA MARIA WA MLIMA KARMELI.**

(Isaliwe siku zote 9 Haibadiliki)

**1.Mwaliko wa Utatu Mtakatifu tukisema kwa Jina  
la Baba na la Mwana na la Roho  
Mtakatifu.Amina**

**2.Sali sala ya Uje Roho Mtakatifu**

**3.Sala kwa Bikira Maria wa Mlima Karmeli**

Ee Ua zuri la Karmeli, mzabibu wenye ukuu sana, Fahari ya mbingu, Mtakatifu na uliye wa pekee, ambaye ulimleta kwetu Mwana wa Mungu, na bado daima unabaki Bikira safi sana.

Unisaidie katika shida hii (Taja nia zako) Ewe Nyota ya Bahari unisaidie na unilinde. Nionyeshe kuwa wewe ni mama yangu. Ee Maria uliyekuwa mimba bila dhambi, Utuombee sisi tunaokukimbilia wewe

- Mama wa pambo la Karmeli-utuombee
- Msimamizi wa wote wanaokufa wamevaa Skapulari-Utuombee.
- Mtakatifu Yosef rafiki wa Moyo Mtakatifu wa Yesu-Utuombee
- Mtakatifu Yosefu Mchumba safi wa Maria-Utuombee
- Mtakatifu Yosef somo wetu-Utuombee.

**Ewe Moyo Mtamu wa Maria, Uwe wokovu wetu.**

**Baba Yetu...Salamu Maria...Atukuzwe**

**4.Sali sala ya Kumbuka Ee Bikira Maria....**

